# MAJI TANZANIA

TOLEO NA 018

OKTOBA- DISEMBA, 2022

# Mhe. Rais Samia awapa kongole watendaji wa Wizara ya Maji





*"Zamani huko nilikuwa na ugomvi na watu wa maji. Kwa sasa watu wa maji ni marafiki zangu kweli kweli. Wizara imebadilika. Taasisi zilizoko chini ya wizara zimebadilika. Kazi inafanywa kwelikweli naomba muendelee hivyo hivyo" Rais Dkt. Samia amesema.*

## DAWASA Yaagizwa kuongeza uzalishaji wa Maji ya visima virefu



# Mhe. Rais Samia awapa kongole watendaji wa Wizara ya Maji






*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizindua mradi wa maji wa Kakonko-Kiziguzigu, pamoja na viongozi na washirika wa maendeleo*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amezindua skimu ya maji ya Kakonko-Kiziguzigu inayotekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Enabel kutoka nchini Ubelgiji.
Skimu hiyo inatekelezwa kwa gharama ya zaidi ya shilingi Bilioni nne na inatarajiwa kunufaisha kata nne za Kakonko Mjini, Kiziguzigu, Kasuga na Kanyonza zenye idadi ya vijiji 14.

Akizungumza na watumishi wa Wizara ya Maji mara baada ya uzinduzi huo Mhe. Rais Dkt. Samia amewapongeza watumishi hao kwa usimamizi mzuri wa miradi ya maji. Amesema mabadiliko chanya yanayoonekana kupitia wizara hiyo yanatoa matumaini kuwa serikali itafikia malengo yaliyokusudiwa katika sekta ya maji.

"Zamani huko nilikuwa na ugomvi na watu wa maji. Kwa sasa watu wa maji ni marafiki zangu kweli kweli. Wizara imebadilika. Taasisi zilizoko chini ya wizara zimebadilika. Kazi inafanywa kwelikweli naomba muendelee hivyo hivyo" Rais Dkt. Samia amesema.



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Nadhifa Kemikimba akitoa maelezo mahusisi kuhusu mradi wa maji wa Kakonko-Kiziguzigu kwa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kabla ya kufanya uzinduzi.*

# DAWASA Yaagizwa kuongeza uzalishaji wa Maji ya visima virefu



Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imetakiwa kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza kazi ya uchimbaji wa visima zaidi ili kuongeza uzalishaji wa maji jijini Dar es salaam ili kukabiliana na changamoto ya ukame.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa kwa viongozi wa DAWASA alipokutana nao pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na Waziri wa Maji kwa lengo la kujadili hali ya upatikanaji wa maji kwa Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani.

Amesema kuwa Serikali itahakikisha maeneo yote yanapata huduma za maji na kuongeza kuwa kazi ya uchimbaji wa visima pamoja na kutafuta vyanzo vingine vya maji inaendelea ili kufikia matamanio ya Serikali ya kufikisha huduma ya maji karibu na makazi ya wananchi.

Mara baada ya kukagua na kuwasha pampu katika mradi wa Visima vya Maji Kigamboni, amesema kuwa visima hivyo vinauwezo wa kuzalisha lita milioni 70 za maji kwa siku vitakavyosaidia katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa maji katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Mnamo Novemba Mosi Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizungumza katika Kongamano la Kitaifa la Nishati Safi ya Kupikia alimuagiza Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa kuhakikisha anasimamia uunganishwaji wa maji kutoka Kigamboni kwenda maeneo ya Jiji la Dar es Salaam ili kupunguza makali ya mgao.

Waziri Mkuu amesema kuwa mahitaji ya maji kwa Dar es Salaam na Pwani ni lita milioni 544 kwa siku, na ambapo DAWASA inazalisha maji lita milioni 520 kwa siku, mbadala wa maji ya visima hasa kwa kipindi hiki ni jambo la msingi sana kwa lengo la kukabiliana na upungufu wa maji.

"Katika kipindi hiki ambacho kiwango cha maji katika Mto Ruvu kimepungua, uzalishaji wa maji nao umepungua na kufikia lita milioni 300 kwa siku, na kusababisha upungufu wa lita milioni 244, hivyo lita milioni 70 zinazoingizwa mjini kutoka katika mradi wa Visima vya Kigamboni, kutakuwa na upungufu wa maji lita milioni 174, hivyo zitasaidia kupunguza changamoto ya maji ya upatikanaji wa maji katika baadhi ya maeneo," ameeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan alitoa shilingi bilioni 25 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa uchimbaji visima 10 katika eneo la Kigamboni, ambapo kati yake visima saba ndio vimewezesha upatikanaji wa lita milioni 70. "Niwatake DAWASA kuendelea na uchimbaji wa visima vingine ili kukabiliana na upungufu wa maji uliopo," amesema.

Pamoja na hilo, Mhe. Waziri Mkuu ameitaka Wizara ya Maji kushirikiana na sekta binafsi katika kuhakikisha inakamilisha taratibu za utekelezaji wa mradi wa kutoa maji Mto Rufiji utakaosambaza maji katika maeneo ya Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam.

Awali, Waziri wa Maji Mhe Jumaa Aweso (Mb) alisema kuwa Wizara imejipanga kikamilifu katika kuhakikisha maji ya uhakika yanaendelea kupatikana jijini Dar es Salaam na maeneo mengine nchini, ambapo Wizara inaendelea kufanya tathmini ya kutumia maji ya ardhini, "kama tumeweza kupata lita milioni 70 kutoka Kigamboni tunaamini tutapata maji mengi zaidi kupitia miradi ya uchimbaji wa visima," Mhe. Aweso ameeleza.

Akizungumza kuhusu mradi wa kutoa maji kutoka Mto Rufiji, Mhe Waziri Aweso amesema Wizara inaendelea na ufutialiji wa mradi huo ambao unatarajiwa kuzalisha lita milioni 750 za maji kwa siku na hivyo kuondoa changamoto ya upatikanaji wa majisafi kwa Dar es Salaam na Pwani.



Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akikabidhi mfano wa funguo kwa Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) na Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Anthony Sanga



Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akikata utepe kuzindua mradi wa maji wa Kigamboni na kugawa mitambo ya kisasa ya kuchimba maji na ujenzi wa mabwawa



Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwasha mashine ili kusukuma maji katika tanki la mradi wa maji wa Kigamboni.



Sehemu ya mitambo ambayo Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameigawa kwa Sekta ya Maji katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma toshelevu ya maji

# Serikali kujenga zaidi ya Miradi 1,000 ya Maji



***Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Anthony Sanga akiongea katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la mradi wa majisafi wa Mbalache-Lupombwe***

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga amesema Serikali inajenga zaidi ya miradi 1,000 katika maeneo mbalimbali kote nchini ili kuwasogezea huduma ya majisafi , salama na ya kutosha wananchi wake.

Mhandisi Sanga amesema hayo wakati wa hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la mradi wa majisafi wa Mbalache-Lupombwe.

“Kila kona ya nchi hii kuna mradi unajengwa na niwahakikishie miradi mingi inayojengwa kipindi hiki ni miradi yenye ubora mzuri na hata kwenye Mbio za Mwenge mwaka huu miradi iliyokaguliwa ilipongezwa na viongozi wa mbio za mwenge,” Mhandisi Sanga amesema.

Mhandisi Sanga amewapongeza wataalam Wizara ya Maji kwa kuhakikisha ubora wa miradi lakini pia aliwapongeza Viongozi wa Serikali na Chama cha Mapinduzi Wilayani Makete kwa jitihada zao, ufuatiliaji na usimamizi wa ujenzi wa miradi ya maji wilayani humo.

## Wataalamu wa Nigeria waja Tanzania Kujifunza



Timu ya wataalamu wanaofanya kazi katika sekta ya maji kutoka nchini Nigeria imefanya ziara hapa nchini kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu kuhusiana na utekelezaji, usimamizi na uendelezaji wa sekta ya maji.

Timu ya wataalamu hao imekuja baada ya kubaini mafanikio makubwa na mageuzi katika sekta ya maji yaliyofanywa na serikali ya awamu ya Sita nchini Tanzania na kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi bora Afrika na Duniani katika utekelezaji wa program mbalimbali zinazohusu sekta ya maji.

# Mamlaka za Maji nchini zatakiwa kuzingatia miongozo inayotolewa na EWURA kuboresha huduma

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Mha. Modestus Lumato amewataka watendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini kuzingatia miongozo mbalimbali inayotolewa na EWURA ili kuboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo yao.

Mha. Lumato ametoa maelekezo hayo, jijini Dodoma wakati akifungua mafunzo kwa watendaji hao, yaliyolenga kuwajengea uwezo katika maandalizi ya mikakati ya utendaji ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma.

“Kama mlivyoelekezwa awali, kuja na mikakati yenu inayozingatia miongozo iliyotolewa na EWURA, mafunzo haya yatawawezesha kuboresha mikakati hiyo itakayoongeza ufanisi wa utendaji wenu” alisisitiza Lumato.

Naye Mkurugenzi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira EWURA, Mha. Exaudi Fatael, ameeleza kuwa, EWURA imeandaa miongozo husika kwa lengo la kuimarisha huduma hususani katika kudhibiti majanga, kudhibiti upotevu wa maji pamoja na namna bora ya kuchagua, kufunga, kupima na kutunza dira za maji sanjari na muongozo wa kushindanisha utendaji wa mamlaka za maji.

Mafunzo yamehudhuriwa na jumla ya watendaji 31 kutoka mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Tabora,Singida,Iringa, Kilimanjaro, Tanga, Manyara na Morogoro kwa kwa siku nne katika ofisi za Makao Makuu ya EWURA jijini Dodoma.



*Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Mha. Modestus Lumato akifungua mafunzo ya siku nne kwa watendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini jijini Dodoma.*



# Taasisi zatakiwa kushirikiana kupunguza makali ya mgao




Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akielekeza matumizi ya mitambo mipya ya kuchimba visima katika kupunguza makali ya mgao wa maji jijini Dar es salaam

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ametaka Taasisi za Wizara ya Maji kushirikiana katika kukabiliana na upungufu wa maji uliolikumba jiji la Dar es salaam wakati wa kiangazi.

Miongoni mwa taasisi hizo ni RUWASA, DAWASA, Bonde la Wami/Ruvu na Chuo cha Maji, ambapo ameelekeza Bonde la Wami/Ruvu kuainisha maeneo yenye uwezekano wa kupata maji chini ya ardhi na visima vya dharura vichimbwe ili kupunguza makali ya mgao wa maji.

Amesema hayo jijini Dar es salaam na kuelekeza visima vilivyochimbwa miaka ya nyuma vipatavyo 197 kazi ya kuvikagua ifanyike na kuviboresha ili vitumike.

Mhe. Aweso ameitaka DAWASA kuunganisha visima vitakavyochimbwa katika mfumo wa usambazaji wa maji ili kuweza kuongeza wingi wa maji.

Aidha, Mhe. Aweso amekagua na kuagiza mitambo mipya ya kuchimba visima kuanza kutumika kwa dharura kabla ya kufanyiwa uzinduzi.

Hivi sasa, pamoja na kazi kubwa ya wataalamu wa sekta ya maji, hali ya huduma ya majisafi katika jiji la Dar es salaam imetengamaa.



# Maji ya kimataifa yatumike kukuza ushirikiano

Waziri wa Maji, Nishati na Madini Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Shahibu Hassan Kaduara amewasisitiza watumiaji wa maji ya kimataifa kuwa waangalifu na wayatumie kwa matumizi sahihi na usawa bila kuathiri watumiaji wengine.

Mhe. Kaduara ameyasema hayo kwa niaba ya Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) wakati akifungua Kongamano la wadau wa maji ya kimataifa lililofanyika jijini Dar es Salaam.

Amesema maji ya kimataifa yanapaswa kutumika kwa namna ambayo itasaidia pande zote ambazo zinachangia maji hayo ili kuleta maendeleo na siyo ugomvi.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Anthony Sanga amesisitiza makubaliano ya pamoja kwa wadau wa maji ya kimataifa ili nchi zinazochangia maji hayo ziwe na makubaliano ya pamoja katika kutekeleza majukumu.

Maji ya kimataifa ni maji shirikishi, yale yanayovuka mipaka ya nchi mfano maji ya ziwa Tanganyika, ziwa Viktoria, ziwa Nyasa na Mto Nile.




*Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Anthony Sanga akiongoza mjadala wakati wa Kongamano la wadau wa maji ya kimataifa, jijini Dar es salaam*

# Wiki ya Maji India

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) akikata utepe kufungua banda la maonyesho ya vifaa na mitambo mbalimbali inayotumika katika kazi za Sekta ya Maji katika maadhimisho ya saba ya Wiki ya Maji ya India yaliyofanyika katika jiji la New Delhi. Pamoja naye ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Nadhifa Kemikimba na viongozi wa Sekta ya Maji wa nchini India.



# Dkt. Mpango ataka miradi ya maji isimamiwe, bei ya nishati ya gesi ipitiwe






Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango ameitaka Wizara ya Maji kufuatilia matumizi ya fedha za miradi ya maji na kuchukua hatua kwa wote ambao wanashindwa kutumia fedha kama ilivyopangwa.

Dkt. Mpango amesema hayo jijini Mbeya wakati wa Mkutano mkuu wa nane wa mwaka wa Bodi za Maji za Mabonde uliofanyika katika hoteli ya Eden, jijini Mbeya.

Mkutano huo umehusisha uzinduzi wa kampeni ya kupanda miti rafiki kwa vyanzo vya maji katika chanzo cha maji cha Nzovwe, na kampeni hiyo itaendelea kitaifa.

Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Mpango amesisitiza miradi ya maji isimamiwe vizuri kwa sababu wananchi wanahitaji maji, hivyo ili kunusuru vyanzo vya maji ni muhimu kubadili tabia za watu kwani wanachangia katika uharibifu wa vyanzo hivyo.

Pamoja na hilo, ameongeza kuwa ipo haja ya kuangalia bei za nishati, ikiwamo gesi ili wananchi waweze kumudu bei yake badala ya kutegemea nishati ya mkaa ambao unachochea ukataji wa miti na kuharibu mazingira.

Mhe. Dkt. Mpango amesisitiza pia ufugaji wa kisasa uwe kipaumbele na wakulima wapimiwe mashamba ya mifugo na sio kuzunguka nchi nzima, kwani mifugo ikizurura inaharibu mazingira.

Pamoja na hayo, ametaka wananchi wote waliojenga katika milima ambayo ni vyanzo vya maji wapatiwe maeneo mengine na wahame katika maeneo hayo.

Amesisitiza suala la utunzaji wa vyanzo vya maji na kuviendeleza ni jukumu la wananchi wote.


WIZARA YA MAJI
HERI YA SIKUKUU YA UHURU WA TANZANIA
61 MIAKA YA UHURU WA TANZANIA
1961-2022
"Tulinde na Tutunze miradi na vyanzo vya maji"
www.maji.go.tz


WIZARA YA MAJI
HERI YA SIKUKUU YA
Noeli
"Tulinde na Tutunze miradi na vyanzo vya maji"


WIZARA YA MAJI
HERI YA MWAKA MPYA
2023
"Tulinde na Tutunze miradi na vyanzo vya maji"



**Kitengo cha Mawasiliano**

Tovuti: www.maji.go.tz